BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 11 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. **WIMBO WA TAIFA.**

II. **DUA.**

III. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 11 Novemba, 2025.

IV. **MASWALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

238. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane imefanikisha Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ufunguaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo Unguja na Pemba.

(a) Je, miradi mingapi ya maendeleo imefunguliwa kwa

Unguja na Pemba

(b) Je, Miradi gani imefunguliwa na Mawaziri.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

152. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mji wa Chake Chake umeshuhudia ongezeko la magari ya abiria, huku kukiwa na ukosefu wa stendi rasmi ya magari ya abiria, jambo linaloathiri upangaji wa usafiri na usalama wa abiria.

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa muda mfupi na wa haraka wa kujenga stendi ya magari ya abiria katika mji wa Chake Chake.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Boara:**

65. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Katika kipindi cha Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2025, Chama cha ACT Wazalendo kilitamka bayana kuwa kiwango cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi kitakuwa ni milioni moja (1,000,000), iwapo wananchi hao wangelikipa ushindi chama hicho. Aidha, Chama cha Mapinduzi (CCM), kilitamka bayana kuwa kitaongeza kiwango cha mshahara hata kama hakikutangaza kiwango maalum cha nyongeza hiyo.

(a) Lini wafanyakazi wetu wategemee kiwango hicho kipya cha mshahara.

(b) Kwa kuzingatia nyongeza ya mshahara kwa kiwango ambacho kitaongezwa, je kiwango cha chini cha mshahara huo kinatarajiwa kuwa cha kiasi gani.

188. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa mujibu wa Mabadiliko ya Muundo wa Utumishi wa mwaka 2010 (Public Service Reform Program 2010), ilielekeza kuwe na mfumo wa urithishaji na ujengaji wa viongozi katika taasisi (Succession Plan).

Je, ni taasisi ngapi za Serikali mpaka sasa zimetekeleza mpango huu muhimu wa Serikali na ni zipi ambazo mpaka sasa hazijaweza kutekeleza mpango huo.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji:</u>**

14. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Serikali inatoa ruzuku yoyote au faida maalum kwa wawekezaji wanaoanzisha miradi ya maendeleo kwa manufaa ya jamii.

81. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la kampuni za nje zinazofanya kazi hapa Zanzibar.

Je, ni kwa namna gani Serikali inatathmini ajira zinazotolewa kwa wazawa kupitia kampuni za nje zinazofanya kazi hapa Zanzibar.

**<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>**

172. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali huandaa hesabu jumuishi za kila mwaka kwa lengo la kuonesha hali halisi ya kifedha ya Serikali katika mwaka husika wa fedha, kama sehemu ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi bora wa rasilimali za umma. Hata

hivyo, kwa sasa Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali hutumia mifumo tofauti ya uhasibu, ikiwemo mfumo wa "*Cash Basis* na *Accrual Basis"* katika kuandaa na kufunga hesabu zao za mwisho wa mwaka wa fedha, hali inayoweza kuathiri ulinganifu, uthabiti na ubora wa taarifa za kifedha za Serikali kwa ujumla.

Kwa nini Serikali haianzishi na kutekeleza mfumo mmoja wa pamoja wa uhasibu kwa ajili ya utayarishaji na ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha kwa Wizara na Taasisi zake zote.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

21. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo ya kisasa kwa wakulima wa Zanzibar na kuboresha mbinu za kilimo zenye tija, ili kupambana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

184. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Jimbo la Ole ni miongoni mwa maeneo yenye migogoro mingi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Mjini Ole, Kwa Pweza na Maeneo ya Makaani ya Vitongoji.

(a) Je, kwa kiwango kipi Serikali inaifahamu migogoro hiyo.

(b) Je, ni zipi juhudi za Serikali za kutatua migogoro katika maeneo haya ndani ya jimbo la Ole.

(c) Je, ni migogoro mingapi ya ardhi imeripotiwa kwa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

140. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu, Serikali imekifunga kisima cha maji kilichopo Gawani Wete, jambo linalowakosesha wananchi wa Wete kupata maji safi na salama na kuleta kero na usumbufu mkubwa.

Je, lini Serikali watakifunguwa kisima cha Gawani ili wananchi waepukane na ndoo kichwani.

226. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tatizo la kuzimwa umeme kila wakati limekuwa sugu katika kipindi cha hivi karibuni na linaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi katika harakati zao za kiuchumi na kijamii.

(a) Je, kuna sababu gani za msingi zinazopelekea umeme kuzimwa mara kwa mara kwa kiwango kikubwa katika kipindi hichi.

(b) Je, kuna njia gani mbadala zimebuniwa ili kuwa na umeme mbadala badala ya kutegemea umeme wa TANESCO.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

68. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kuwajali wazee wetu wa miaka ya 70, ameamua kuwapa pencheni kwa kila mwezi.

(a) Kuna usahihi upi wa nadharia kwamba, baadhi ya wazee wametimia miaka inayotakiwa, lakini hawapewi pencheni hiyo.

(b) Je, Serikali hutumia vigezo gani kuwapa wazee pencheni ya kila mwezi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

199. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali inahimiza dhana ya wananchi kujiari wenyewe ili kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira hapa nchini. Kwa kuwa katika kisiwa cha Pemba ukulima wa zao la mwani ni moja wapo ya shughuli inayowaingizia watu kipato.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani ya kutoa elimu ya zao hilo kwa wananchi wa jimbo la Mkoani haswa kwa wale wanaoishi katika visiwa vilivyopo katika jimbo hilo.

(b) Je, Serikali inawahakikishia vipi wakulima hao kupata soko la uhakika la mwani unaozalishwa katika jimbo la Mkoani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

2. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa skuli zote za Serikali zinakuwa na huduma za kwanza ili wanafunzi waweze kuhudumiwa mara tu wanapopata tatizo la kiafya.

50. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza elimu bila ya malipo ambayo maana yake ni asilimia mia moja ya wananchi wa Zanzibar walipata elimu ya msingi hadi sekondari na hata vyuo vikuu bure bila ya malipo wala michango yoyote ya kifedha. Hata hivyo, hivi sasa katika skuli za Serikali nchini kote, wanafunzi huchangia michango mbali mbali ambayo, japo ni kweli kuwa sio sawa na kuilipia elimu, lakini sio bure ya asilimia mia moja kama ilivyokuwa imetangazwa mwaka 1964.

(a) Kwa nini Serikali bado inasimamia elimu bila ya malipo hapa Zanzibar wakati ni tofauti na uhalisia uliopo.

(b) Ni lini neno 'Elimu bila ya Malipo' litabadilishwa katika sera au moto za skuli zetu na badala yake ikawa elimu inayochangiwa.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

161. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuboresha na kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo tofauti ya nchi kwa lengo la kuboresha usafiri na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Pamoja na jitihada hizo, barabara ya Mapinduzi iliyopo katika mji wa Chake Chake Pemba, bado haijajengwa kwa kiwango cha lami licha ya kuwekewa ahadi muda mrefu.

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

181. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Sehemu kubwa ya wananchi wa jimbo la Ole wanaoishi Uwandani, Vitongoji na Mjini Ole, wanategemea zaidi kilimo kuwaingizia kipato, huku wakikabiliwa na changamoto za kukosekana kwa barabara za ndani za kuweza kufika katika shughuli zao za maendeleo.

(a) Ni lini Serikali itazijenga barabara zinazotoka Ole kuelekea Shumindu; Kangagani kuelekea Kwareni Makaani; Dodeani Kilimo kupitia Uwandani hadi Makaani na barabara ya Vitongoji kuelekea Makaani hadi Kwareni.

(b) Je, ni ipi tathmini ya ujenzi wa barabara za ndani kwa kilomita (KM) kwa kila jimbo katika majimbo 50 ya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

121. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kwa kuwa Serikali inatoa mikopo kwa wajasiriamali na kina mama.

Je, ni vikundi vingapi vilivyopatiwa mikopo katika Mkoa wa Kusini Pemba kwa kipindi cha miaka miwili hii.

## V. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

**Zanzibar,**
**11 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**